JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na:*025-2802318/2802137*
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA MKOA WA RUKWA KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI MACHI, 2021 HADI JANUARI, 2024

1.0. HISTORIA YA MKOA WA RUKWA

Ndugu Wanahabari,Mkoa wa Rukwa ulianzishwa Mwaka 1974 kwa kumega sehemu ya Mkoa wa Tabora (Wilaya ya Mpanda) na Mbeya (Wilaya ya Sumbawanga). Mnamo mwaka 2010 mwezi Julai Serikali iliamua kumega Wilaya ya Mpanda na kuanzisha Mkoa mpya wa Katavi. Mkoa unapakana na Mikoa ya Katavi (upande wa Kaskazini na Songwe upande wa Mashariki). Aidha, unapakana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Upande wa Magharibi).

1.1. Muundo wa Kiutawala

Mkoa una jumla ya Wilaya tatu (3) ambazo ni Sumbawanga, Kalambo na Nkasi na Halmashauri nne (4) ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Nkasi na Kalambo. Aidha, ndani ya Mkoa kuna Mamlaka za Miji Midogo za Namanyere Wilayani Nkasi na Laela Wilayani Sumbawanga. Yapo majimbo matano (5) ya Uchaguzi ambayo ni Sumbawanga Mjini, Kwela, Kalambo, Nkasi Kusini na Nkasi Kaskazini. Mkoa una Tarafa 16, Kata 97, Vijiji 339, Vitongoji 1,817 na Mitaa 165.

2.0. ENEO NA IDADI YA WATU

Mkoa wa Rukwa una eneo la Kilometa za Mraba **27,765** kati ya hizo Kilometa za mraba **22,844**(**82.3%**)ni za nchi kavu na Kilometa za mraba **4,921**(**17.7%**)ni za maji.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Mkoa wa Rukwa umekuwa na idadi ya watu **1,540,519**(Wanaume **743,119**) na (Wanawake **797,400**) wastani wa ongezeko la idadi ya watu ni **4.3.**

2.1. PATO LA MKOA

Ndugu Wanahabari,Uchumi wa Mkoa unategemea kilimo, uvuvi, ufugaji, uchimbaji wa madini, biashara, uzalishaji viwandani na ajira katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi. Pato la Mkoa kwa mujibu wa Takwimu za NBS limekuwa likiongezeka kila mwaka ambapo mwaka 2016 lilikuwa milioni **2,518,000** Mwaka 2018 lilikuwa milioni **2,753,744.4** na 2021 lilikuwa milioni **3,470,996.2** na mwaka 2022 lilikuwa milioni **3,588,000.** Kwa upande wa pato la mtu mmoja mmoja pia limeongezeka na kufikia Shilingi **2,329,098**Mwaka 2022.

3.0. MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 HADI 2023/2024

3.1. Utekelezaji wa miradi ya sekretarieti ya Mkoa

3.1.1. Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi

Ndugu Wanahabari,Kutokana na uchakavu wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitoa kiasi cha shilingi **1,429,498,810.06**kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi ambapo ujenzi wa Ofisi hiyo umefikia asilimia 70. Tunamshukuru sana Mhe. Rais

kwakujenga Ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya kama sehemu ya kuboresha utawala bora kwani Ofisi iliyokuwepo ilikuwa ni chakavu sana.

3.1.2. Ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Kalambo.

Ndugu Wanahabari,Wilaya ya Kalambo haikuwa nanyumba ya Mkuu wa Wilaya. Kutokana na hali hiyo Serikali ilitoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni**1,000,000,000.00** nakutumia shilingi **950,000,000.00 (**ambapo shilingi**873,216,035.69** zimelipwa kwa Mkandarasi SUMA JKT na shilingi**76,783,964.31**kwa Mtaalam Mshauri -TBA**)** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Kalambo ambayo tayari imekamilika isipokuwa shughuli ndogondogo hazijakamilika ikiwemo kutengeneza mazingira ya nje ”*Land scapping*”. Haya ni mafanikio makubwa sana katika kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wanakuwa na nyumba.

4.0. MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KATIKA HALMASHAURI

4.1. Elimu ya Awali

Ndugu Wanahabari, Mkoa wa Rukwa una jumla Shule za Msingi **379** zenye Madarasa ya Elimu ya Awali, ambapo kati ya hayo yaliyopo kwenye shule za Serikali ni **366** na yaliyopo kwenye shule zisizo za Serikali ni **13.** Hadi kufikia tarehe 25 Januari, 2024 Mkoa umeongeza Shule zenye Madarasa ya Elimu ya Awali kufikia Shule za Msingi **399**.

Ndugu Wanahabari, mwaka 2024, tulitarajia kuandikisha Wanafunzi wapya **57,006**waElimu ya Awali(Wavulana **27,885** na Wasichana **29,121**) ambapo kufikia Januari 25, 2024 tumeandikisha wanafunzi **36,753** wa Darasa la Elimu ya Awali (Wavulana **18,222** na Wasichana **18,531).** Kati ya wanafunzi walioandikishwa, walioripoti ni Wanafunzi

32,932 (Wavulana **16,251** na Wasichana **16,681)** wakiwemo wanafunzi **49** wenye mahitaji maalum sawa na asilimia **89.6.**

4.2. Elimu ya Msingi Darasa la I – VII

Ndugu Wanahabari, Mwaka 2021 Mwezi Machi Mkoa wa Rukwa ulikuwa na shule za Msingi **379** ambapo Shule za Serikali zilikuwa **366** na shule **13** zisizo za Serikali. Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 Shule za Msingi zimeongezeka hadi kufikia **409** ambapo za Serikalini**392** na Zisizo za Serikali ni **17**sawa naongezeko la asilimia **7.9**.

Ndugu Wanahabari, mwaka 2024 tulitegemea kuandikisha wanafunzi wapya **51,347** wa darasa la Kwanza, **(**Wavulana **25,254** na Wasichana **26,093),** ambapo hadi kufikia tarehe 25 Janauri, 2024 tumeandikisha wanafunzi **43,069** (Wavulana **20,923** na Wasichana **22,146**) sawa na asilimia **83.9.** Kati ya wanafunzi hao, wenye mahitaji maalum ni wanafunzi **53**. Aidha, ufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ulikuwa asilimia **78.30** Mwaka 2023.

4.3. Elimu ya Sekondari

Ndugu Wanahabari, Mkoa wa Rukwa mwaka 2021 ulikuwa na Shule za Sekondari **97** ambapo Shule za **Serikali** zilikuwa **73** na Shule **Zisizo za Serikali** ni **24.** Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 Mkoa wa Rukwa una jumla shule za Sekondari **112** ambapo za **Serikali** ni **85** na **Zisizo za Serikali** ni **27.** Jumla ya wanafunzi wapya **24,409** (Wavulana **11,312** na Wasichana **13,097**) wamepangwa kujiunga na Elimu ya Sekondari Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2024. Hadi kufikia Januari 25, 2024 jumla ya wanafunzi **15,684** (Wavulana **7,393** na Wasichana **8,291)** wameripoti shuleni wakiwemo wanafunzi **14** wenye mahitaji

maalum.Ufaulu wa watahiniwa wa Kidato cha Nne umeongezeka kutoka asilimia **87.7** mwaka 2020 hadi asilimia **90.0** mwaka 2023.

5.0. MIRADI YA UJENZI SEKTA YA ELIMU

Ndugu Wanahabari,kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 Mkoa wa Rukwa umepokea Shilingi **64,706,952,025.24** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu. Kati ya fedha hizo shilingi **41,228,532,481.03**kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari ambapo miundombinu ya Elimu ya Awali zilipokelewa shilingi **1,121,596,000.00** Elimu ya Msingi **14,105,282,369.03** na Elimu ya Sekondari shilingi **26,001,654,112.00** kwa upande wa vyuo vya kati na vyuo vikuu zilipokelewa shilingi **23,478,419,544.21.**

Aidha, kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 Mkoa ulipokea Shilingi bilioni **27,646,322,946.21** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Sekta ya Elimu. Miradi iliyotekelezwa kutokana na fedha hizo ni pamoja na ujenzi wa shule mpya za msingi na Sekondari, vyumba vya madarasa, mabweni, matundu ya vyoo na maabara.

5.1. Shule ya Mkoa ya Wasichana

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea kiasi cha shilingi **3,000,000,000.00**kwa ajili ya ujenzi wa shule ya Mkoa inayojengwa katika eneo la Laela Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Ujenzi wa shule hiyo umefikia asilimia **85.**

5.2. Mradi wa BOOST

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea shilingi **6,064,900,000.00**kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za msingi 9, madarasa ya Elimu ya awali 26,

madarasa ya shule za msingi 150, matundu ya vyoo 251, nyumba 2 za walimu na ukarabati wa shule kongwe 1. Miradi hiyo imekamilika na inatumika.

5.3. Mradi wa SEQUIP

Ndugu Wanahabari, Katika kipindi cha miaka 3 Mkoa ulipokea shilingi **6,336,170,140.00** kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya 11 na nyumba 6 za walimu.Awamu ya kwanza zilipokelewa shilingi **2,820,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya sita (6) za Sekondari katika kata za Mnamba, Paramawe, Kizumbi, Nankanga, Laela na Momoka na Awamu ya Pili zilipokelewa shilingi **2,916,170,140.00** ambazo zilitumikakujenga shule tano za Sekondari za Kata za Chanji, Ntatumbila, Kalumbaleza, Ninde na Mpombwe. Pia zilipokelewa **600,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 6 za walimu (Two in One) katika kata hizo. Shule 10 kati ya 11 zimekamilika na Wanafunzi wanasoma isipokuwa shule ya Sekondari Kalumbaleza ambayo bado haijapangiwa Wanafunzi.

5.4. VYUO VYA KATI NA ELIMU YA JUU

5.4.1 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Tawi la Rukwa

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea kiasi cha Shilingi **14,679,637,854.00**kwa ajili ya Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Tawi la Rukwa ambapo panajengwa Jengo la Taaluma ambalo litakuwa na ofisi za wafanyakazi, vyumba vya mihadhara, maktaba na maabara. Pia ujenzi utahusisha majengo ya karakana na barabara kuzunguka majengo. Ujenzi unaendelea vizuri.

5.4.2 Ujenzi wa Chuo cha VETA Sumbawanga

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka mitatu Mkoa ulipokea Shilingi **2,412,916,381.97**kwa ajili ya umaliziaji wa Chuo cha VETA

Sumbawanga. Utekelezaji wa mradi umefikia **98%**, kazi zinazoendelea ni ukamilishaji wa bweni moja na nyumba ya Mwalimu.

5.4.3 Ujenzi wa Chuo cha VETA Paramawe

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea Shilingi Milioni **348,412,790.23**kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa, bwalo, jiko na matundu ya vyoo katika chuo cha VETA Paramawe, utekelezaji wa ujenzi upo katika hatua ya upauaji majengo.

5.4.4 Ujenzi wa Chuo cha VETA Kalambo

Ndugu Wanahabari, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mkoa ulipokea Shilingi **324,694,243.01** kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Kalambo. Chuo kitakuwa na miundombinu ya majengo ya karakana, jengo la utawala, madarasa, vyoo, nyumba ya Mkuu wa Chuo na nyumba ya mlinzi. Mpaka sasa hatua ya utekelezaji majengo ya karakana yapo hatua ya msingi (kumwaga jamvi) na majengo ya madarasa, utawala, mlinzi, vyoo na nyumba ya mkuu wa chuo yapo hatua mbalimbali za kujenga ukuta.

5.4.5 Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea kiasi cha Shilingi **1,440,391,727.00**kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya Chuo na ununuzi wa fenicha. Mradi uko katika hatua ya ukamilishaji wa bweni uwekaji wa tarazo na kupaka rangi.

6.4.6 Ujenzi wa Chuo cha Ualimu cha Sumbawanga

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha miaka mitatu, Mkoa ulipokea Shilingi **4,272,366,548.00**kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kipya cha Ualimu Sumbawanga ambapo tulikuwa tunatumia majengo ya Kanisa Katoliki Sumbawanga. Kuletwa kwa fedha hizo na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Mkoani kwetu zimewezesha Chuo hicho kuhamia katika

majengo yao mapya na kutoka katika majengo ya Kanisa. Kwa niaba ya Wanarukwa tunamshukuru sana Mhe. Rais kwani chuo hicho kilikuwa kimekaa kwenye majengo ya Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka 30.

5.5. Upanuzi wa Chuo cha Maafisa Tabibu Sumbawanga

Mkoa ulipokea Shilingi Bilioni **2,300,000,000.00**kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Maafisa Tabibu Sumbawanga. Ujenzi huo utaanza hivi karibuni.

5.6. Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Nyumba ya Mkurugenzi.

Ndugu Wanahabari, Tulipokea shilingi Bilioni 3, 150,000,000 kwaajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na nyumba ya Mkurugenzi. Jengo la Mkurugenzi liligharimu shilingi Bilioni 3,000,000,000 na nyumba ya Mkurugenzi iligharimu shilingi Milioni 150,000,000. Tayari Jengo pamoja na nyumba zimekamilika. Hii imewezesha kuimarika kwa utoaji wa huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ukizingatia kuwa Halmashauri hii ni Mpya.

5.7. Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na Nyumba ya Mkurugenzi

Tulipokea pia shilingi Bilioni 4,323,444,741.28 kwaajili ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo Pamoja na Nyumba ya Mkurugenzi. Jengo la Ofisi liligharimu shilingi Bilioni 4, 4,123,444,741.28na nyumba iligharimu shilingi Milioni 200,000,000. Miradi hiyo tayari imekamilika na inatumika,

6.0. SEKTA YA AFYA, LISHE NA USTAWI WA JAMII

Ndugu Wanahabari, Mwaka 2021 Mkoa wa Rukwa ulikuwa na Hospitali **6**Vituo vya Afya **23** na Zahanati **205.** Hadi kufikia mwezi Januari, 2024

vituo vya kutolea huduma za Afya vimeongezeka ambapo Hospitali za Wilaya zipo **6,** Vituo vya Afya **28** Na Zahanati **217** Kati ya vituo hivyo vya kutolea huduma za Afya vya Serikali ni **220** na Binafsi **34.**

6.1. Miradi ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea Shilingi bilioni **13,770,000,000**kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali za Wilaya za Sumbawanga, iliyopo Mtowisa, Nkasi, Kalambo na Manispaa ya Sumbawanga. Aidha, shilingi bilioni **9,400,000,000.00**. Zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya **21** na Zahanati **30**

Vifaa Tiba Hospitali ya Mkoa, Wilaya na Vituo vya Afya

Ndugu Wanahabari, Mkoa wa Rukwa ulipokea Shilingi **2,900,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Hospitali za Wilaya na Zahanati.

6.2. Ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea Shilingi Bilioni **2,573,770,600.00**kwa mwaka wa fedha 2021/2022 – 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Fedha hizo zimetumika kujenga majengo yafuatayo:- Jengo la Wagonjwa wa dharura, Nyumba ya Mtumishi, Ununuzi wa CT – Scan, Jengo la kutunzia CT – Scan na Uwekaji wa Mfumo wa Telemedicine.

7.0. SEKTA YA MAJI

7.1. Maji vijijini (RUWASA)

Ndugu Wanahabari, Mkoa ulipokea Shilingi Bilioni **29,200,000,000.00**kwa ajili ya miradi ya maji vijijini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024. Fedha hizo zimetekeleza miradi **51** ya maji. Baada ya kutekeleza miradi hiyo asilimia ya

upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka na kufikia asilimia **64** mwezi Januari, 2024.

7.2. Maji mjini (SUWASA)

Ndugu Wanahabari,Katika kuhakikisha kuwa Serikali inaboresha mtandao wa upatikanaji wa maji Mjini Sumbawanga, jumla ya Shilingi Bilioni **2,600,000,000.00** zilitolewa kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maji Manispaa ya Sumbawanga. Kazi hiyo tayari imekamilika na wananchi wanapata maji. Fedha hizo zilizotolewa zimeongeza asilimia ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia **86**Mwaka 2020 hadi asilimia **93** Mwezi Januari, 2024.

8.0. MIUNDOMBINU YA BARABARA

8.1. Barabara za TANROADS

Ndugu Wanahabari, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 TANROADS imepokea Shilingi Bilioni **11,840,000,000.00**kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa Barabara. Barabara zote za TANROADS zinapitika japokuwa katika kipindi hiki cha mvua baadhi ya barabara zimeharibiwa na mvua.

8.2. Ujenzi wa Barabara ya Ntendo – Muze sehemu ya Ntendo – Kizungu na Matai – Kasesya

Ndugu Wanahabari,Mkoa waRukwa ulipokea kiasi cha Shilingi bilioni **45,000,000,000.00** Kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Ntendo – Muze sehemu ya Ntendo Kizungu. Aidha, Shilingi Bilioni **38,000,000,000.00**zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Matai – Kasesya sehemu ya Matai – Tatanda. Miradi hiyo inaendelea na kwasasa Barabara ya Ntendo – Kizungu ipo asilimia **41** ya utekelezaji na Barabara ya Matai-Tatanda ipo asilimia **34** ya utekelezaji.

8.3. Barabara za TARURA

Ndugu Wanahabari,Bajeti ya TARURA katika Mkoa wetu mwaka 2020/2021 ilikuwa Shilingi Bilioni **5,043,637,390.63**lakini bajeti hiyo imeongezeka hadi kufikia Shilingi Bilioni **11,540,000,000.00** Mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 TARURA ilipokea Shilingi Bilioni **25,420,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mjini na Vijijini ili kuimarisha shughuli za usafiri na usafirishaji

8.4. Mradi wa TACTIC

Ndugu Wanahabari, Mkoa katika mwaka wa fedha 2023/2024 umepokea zaidi ya Shilingi Bilioni **27,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami Km **13** Mjini Sumbawanga pamoja na ujenzi wa soko la mazao katika eneo la Kanondo. Barabara hizi zikikamilika zitasaidia kuimarisha mandhari ya Mji wetu wa Sumbawanga na kuzifanya zipitike kwa urahisi. Aidha, soko la mazao litawasaidia wakulima kuwa na eneo moja la kuuzia mazao yao na kuwasaidia wasilanguliwe.

9.0. NISHATI

Ndugu Wanahabari, hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wetu ni nzuri. Aidha,kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TANESCO walitengewa Bajeti ya Shilingi Bilioni **45,000,000,000.00**kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umeme wa REA ambapo mpaka kufikia mwezi Januari, 2024 jumla ya Vijiji**292** Vilikuwa vimewashiwa umeme kati ya vijiji**339, Vijiji 47** vinaendelea kuwekewa umeme katika awamu hii na Mkandarasi yupo site. Aidha, wananchi wanaopisha ujenzi wa Gridi ya Taifa walilipwa Shilingi Bilioni **3,380,000,000.00** wakiwemo wananchi kutoka Halmashauri ya Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

10.0. UJENZI WA UWANJA WA NDEGE SUMBAWANGA

Ndugu Wanahabari, Mkoa umekwisha pokea kiasi cha shilingi bilioni **8,000,000,000.00**kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga ambao gharama ya mradi ni jumla ya shilingi bilioni **60,100,000,000.00**Mkandarasi tayari yupo saitianaendelea na ujenzi.

11.0. KILIMO

Ndugu Wanahabari, Mkoa wa Rukwa ni Mkoa wa Kilimo. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka Tani **1,079,809** mwaka 2021/22 hadi tani **1,469,716** mwaka 2022/2023. Hii imetokana na Serikali kuleta Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa Wakulima ambayo imeongeza tija katika uzalishaji. Katika mwaka 2023/2024 Mkoa unatarajia kuzalisha jumla ya Tani **1,654,840**. Hii ni kutokana na hali ya mazao mashambani kuwa ni ya kuridhisha.

11.1. Kilimo cha umwagiliaji

Ndugu Wanahabari,Mkoa ulipokea Shilingi Bilioni **21,000,000,000.00**kwa ajili ya ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Ilemba Halamshauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Mradi huo unaendelea kutekelezwa na umefikia asilimia **15** ya utekelezaji.

12.0. Ukamilishaji wa Bandari ya Kabwe

Ndugu Wanahabari, Jumla ya Shilingi Bilioni **7,400,000,000.00** zilitolewa kwaajili ya kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Kabwe. Ujenzi huo tayari umekamilika na Bandari inafanya kazi. Kukamilika kwa Bandari hiyo kumerahisisha Biashara kati ya Tanzania na Nchi za Congo DRC na Burundi na hivyo kuongeza Mapato ya Kodi mbalimbali kwenye Nchi yetu.

13.0. Bandari ya Kasanga.

Ndugu Wanahabari, Shilingi Bilioni 4,700,000,000.00 zilitolewa kwaajili ya upanuzi wa Bandari ya Kasanga. Mradi huo upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji ambapo tayari Shughuli za Bandari zinaendelea katika Bandari hiyo. Kukamilika kwa Bandari hiyo kutasaidia kuongeza Biashara kati ya nchi ya Tanzania na Congo DRC na Zambia.

Ndugu Wanahabari,Yapo mengi ambayo yametekelezwa katika Mkoa wetu katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu na Wananchi wa Rukwa wanashuhudia maendeleo makubwa.

Kwa niaba ya Wanarukwa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan rais wetu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wa kishindo wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Wanarukwa hatuna cha kumlipa zaidi tunaahidi kumlipa kwenye sanduku la kura.

Mungu Ibariki Tanzania
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa.
Asanteni sana kwa kunisikiliza.

CHARLES MAKONGORO NYERERE
MKUU WA MKOA WA RUKWA